# KILIMO MSITU

## Njia Bora Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

### Kujengea Jamii Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Upandaji Miti








### Kwa Nini Mabadiliko ya Tabianchi ni Muhimu kwa Wakulima?

- Mvua haieleweki tena
- Rutuba ya udongo kushuka
- Wadudu na magonjwa yanaongezeka
- Mavuno yanapungua, kipato na chakula vinaathirika



### Kilimo Msitu ni Nini?

Kilimo msitu ni utaratibu wa kupanda miti shambani pamoja na mazao, ili kuongeza uzalishaji, kulinda mazingira, na kujenga ustahimilivu.


### Faida za Kilimo Msitu

- Hurejesha rutuba ya udongo
- Hutoa kivuli na kuhifadhi unyevu
- Hutoa matunda, kuni na kipato
- Husaidia viumbe hai wengine
- Malisho ya mifugo
- Hupunguza mmomonyoko wa ardhi na mafuriko

**ANZA SASA !**

- **Jifunze jinsi kilimo msitu kinavyoweza kubadilisha shamba lako**
- **Jiunge na kikundi cha wakulima kilicho jirani**
- **Muulize Afisa Ugani wa Kijiji jinsi ya kuanza**

Kama utahitaji kufahamu au kupata msaada zaidi wa mafunzo ya mbinu za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, wasiliana na NADO

**Piga Simu: 0756 000 387/0763 204 364/0758 156 477 Baruapepe: info@nado.or.tz**

YouTube: NJOMBE AGRICULTURAL DEVELOPMENT ORGANIZATION

Instagram: nado_tanzania

Facebook: NJOMBE AGRICULTURAL DEVELOPMENT ORGANIZATION

www.nado.or.tz

NJOMBE AGRICULTURAL DEVELOPMENT ORGANIZATION — NADO — UBIA · UMOJA

# Matokeo Muhimu
## utafiti uliofanywa na
# Mradi wa FORI

- Miti kama **Lucina, Secibania Mpogolo, Gliricidia** huota vizuri pamoja na mazao
- Wakulima **waliotumia kilimo msitu** walipata udongo bora zaidi
- Waliongeza **ustahimilivu dhidi ya ukame**
- Waliboresha **usalama wa chakula** na **kipato cha familia**





"Tangu niliposhauriwa na NADO kuchanganya miti rafiki na mazao na kupanda katika mashamba yangu, mazao yameongezeka na udongo unahifadhi unyevu kwa muda mrefu."

*- Fatuma Mgaya, Mkulima, Kijiji cha Wanging'ombe, Njombe*

## Mambo ya Kuzingatia Unapoanza Kilimo Msitu:

- **Anza kidogo:** Chagua miti michache na ipande pembezoni mwa shamba
- **Changanya kwa uangalifu:** Tumia miti na mazao yanayosaidiana
- **Simamia vizuri:** Tifua na kata matawi ili kuepuka kivuli kingi
- **Jiunge na vikundi:** Jifunze kutoka kwa wakulima wenzako na wataalamu

**Kuhusu Mradi wa FORI:**
Mradi wa Utafiti na Ubunifu Unaoongozwa na Wakulima (FORI) unalenga kuwawezesha wakulima hapa Tanzania kwa kutumia tafiti, ubunifu na mbinu endelevu za kilimo ili kujenga ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Ukiongozwa na NADO, kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) na kufadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na OACP kupitia shirika la AGRICORD na FFD, mradi huu unalenga kudhibiti mabadiliko ya tabianchi kupitia upandaji miti.

**Kujengea Jamii Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Upandaji Miti**

Mradi umefadhiliwa na:

Mradi umetekelezwa na:

Kipeperushi hiki kimetayarishwa kwa ufadhili kutoka Umoja wa Ulaya (EU) na OACPS. Maoni yaliyomo kwenye kipeperushi hiki hayaakisi maoni rasmi ya Umoja wa Ulaya (EU) au OACPS.

A5 Flyer Agroforestry.indd 2 8/21/2025 9:21:23 PM